# Learning by Ear – Religious Dialogue: "A Bridge over Gori"

# Episode 06: "Mikono iliyoteketea"

**Author: Romie Singh**

**Editors: Katrin Ogunsade, Naïma Guira**

**Proof reading: Natalie Glanville-Wallis**

**Expert on African religions: Jean-Félix Belinga Belinga**

**KISUAHELI ERIC PONDA/THELMA MWADZAYA**

**List of characters for episode 6:**

- Narrator /Philip, male (17)
- Harry, male (17)
- Layla, male (16)
- Hassan, male (12)
- Ishmail Omer (Layla's father), male (43)
- Sister Rebecca, female (28)
- Marian Okru, female (16)
- Chief Dembele (Harry's father), male (51)
- + Students in the background

1. **SIG TUNE UP**

2. **INTRO:**

**Hujambo na karibu kwa sehemu ya sita ya mfululizo wa Vipindi vya NOA BONGO-Jenga Maisha Yako katika mchezo wa Redio wa DARAJA LA GORI, Hadithi ya kusisimua inayoelezea jinsi Siasa na Dini zinavyoweza kusababisha uhasama baina ya Jamii, na Familia mbili za Mji wa Gori na kadhalika vijana wawili Harry na Layla wanaolazimika kulificha penzi lao.Katika makala ya leo Hassan,mdogo wake Layla anakataa kutumia dawa zake naye Harry anajaribu kuisawazisha hali ambayo tayari imevurugika.Na kama kawaida Philip,mmoja wa wandani wa Harry ndiye anayekusimulia kisa chote.Baki papo hapo!**

3. **PHILIP/NARRATOR:**

**Habari za tukio la usiku huo mjini Gori zilichapishwa kwa kina kwenye Gazeti maarufu mjini humo.Ukurasa wa kwanza wa Gazeti hilo uliandika,"Kanisa jengine lateketea" .Kama mhariri mkuu, Babangu alihakikisha kuwa hayo ndiyo yaliyoandikwa. Hassan amelazwa hospitalini, hali yake taabani kwasababu ya majeraha ya moto.Hata hivyo kwasababu ya umri wake wa miak 12 Gazeti hilo lilikuwa na wajibu wa kulibana jina lake. Lakini kila mmoja alimfahamu mhusika mkuu. Maafisa wa polisi walikuwa wamkisubiri Hassan apate nafuu kisha wamkamate**.T

**Taarifa hizo zilimshtua sana Babake hata akashindwa kumuelewa mwanawe. Hassan kwa upande wake alikuwa anamhitaji mamake sana wakati huo.Kutokana na hilo dadake Layla alilazimika kulijaza pengo hilo kwahiyo akaomba apewe nafasi ya kutohudhuria masomo yake chuoni .**

**<u>Scene 1. In hospital</u>**

**Sister Rebecca, Mr Omer, Layla, Hassan**

**4. <u>SFX: hospital room, monitor peeping, low voices of other patients in the background</u>**

**5. SISTER REBECCA: Bw Omer, Naitwa Rebecca, muuguzi katika hospitali hii. Mtoto wako amekataa dawa na chakula na ndio sababu nikamweka mpira wa kudondosha chakula kwenye mishipa yake ya damu.**

**6. MR OMER: Anatusikia tukizungumza?**

**7. SISTER REBECCA Sidhani. Nafikiri hataki tu kushirikiana nasi wakati tunapojaribu kumsaidia.**

**8. LAYLA: *(whispering)* Hassan, tafadhali zungumza….. Mikono yako imechomeka vibaya..!. Tunataka kukulisha, fungua macho tafadhali.**

**9. HASSAN:** *(whispering)* **Allah atukuzwe…..! Lakini sio na makafiri.**

**10. SISTER REBECCA:** *(gently)* **Nafikiri maneno hayo yananilenga mimi- mimi ni myahudi; Hebu tumpe nafasi kidogo apumzike. Mpira huu utamsaidia kurejesha maji mwilini.**

**11. MR. OMER:** *(desperate)* **Pole sana sister… Lakini alipata wapi mawazo hayo yote? Haya si mafundisho ya Qur'an tukufu….!? Hassan nisikilize mwanangu!**

**12. SISTER REBECCA: Shhhh, Bw Omer, unajisumbua roho na kumkera mgonjwa wangu.. na hata mimi pia..!. Hebu tumuache apumzike. Anahitaji kupumzika tafadhali.**

**13. MR OMER: Layla, tafadhali utalazimika kukaa naye kitandani. Mimi nataka kwenda kazini. Anamhitaji mlezi wa kike zaidi wakati huu** *(crying).* **Msaidie tafadhali apate fahamu zake…!.**

**14. <u>BRIDGING MUSIC</u>**

**15. PHILIP/NARRATOR: Wakati nilipomuona Harry Chuoni kesho yake,alikuwa amejawa hofu na fikra alizokuwa nazo ni kuwa mwisho wa mambo ulikuwa umewadia.Babake mdogo anailaumu Familia ya Omer na tayari alishampiga marufuku kutangamana na Layla nje ya mazingira ya shule.Harry alidai kuwa vijana katika chuo cha Madrassa walimtumia Hassan kufanya uhalifu huo.... masikini mtoto wa watu!Babake mdogo hakutaka kulisikia la muadhini wala mteka maji msikitini.Harry alitutazamia mie na Mat kumsaidia.Zaidi wasiwasi wake ulikuwa kwa Layla, lakini yeye alimtazamia Harry amfariji.**

**<u>Scene 2. Exterior - In school gardens</u>**

**Harry (normal voice), Layla (telephone voice)**

**16. <u>ATMO: birds, students voices, children playing in the background</u>**

**17. <u>Cell phone hooting</u>**

**18. HARRY:** ***(on the phone)*** **Layla? Layla? Nini kinachoendelea,? Uko salama ?**

**19. LAYLA:** **(sobbing) Harry? Ni wewe? Sijui nikwambie nini… ! Samahani sana..!. Na pia umsamehe mdogo wangu Hassan…ni …ni….**

**20. HARRY:** **Layla, Na wewe mwenyewe? Uko salama? Tunaweza kukutana baadaye… Ningependa kuzungumza na wewe Layla!**

**21. LAYLA:** ***(sobbing)*** **Hapana, niko peke yangu nyumbani. Sitaweza kukuona.!**

**22. HARRY:** **Layla, tafadhali,….! nataka kuongea japo kwa dakika tano tu chini ya lile Daraja la Mto Gori?**

**23. LAYLA:** La hasha **Harry ….siwezi!.**

**24. HARRY:** **Hakuna atakayetuona: KWA DAKIKA TANO TU Layla.. tafadhali!**

**25. LAYLA:** **Sawa basi kwa dakika tano tu.. Harry!.**

**26. PHILIP/NARRATOR: Harry alitaka Mimi na Mat tumstiri, maana hangeweza kuhudhuria mazoezi ya kandanda. Alisema kuwa ni wajibu wao yeye na Layla kama viranja wa chuo, kufana kila wawezalo kuumaliza uhasama baina ya familia zao mbili. Mimi na Mat tulitazamana tu.Tulifahamu kwamba kulikuwa kuna mengi zaidi ya hayo.**

**Scene 3. Under Gori Bridge**

**Harry, Layla**

**27. SFX: Street noise, cars passing by, River flowing, birds**

**28. HARRY: Layla, Unadhani utarudi lini shuleni?**

***29.* LAYLA: Hassan hajapata nafuu na anakataa kunywa dawa.Lazima nikae naye hospitalini. Nina hakika ametiwa itikadi kali…!; Nimeisoma barua moja aliyoiandika- kwamba anataka kwenda kuungana na Marehemu Mamangu peponi… Ohh maskini Harry! *(crying)***

**30. HARRY: Oh Layla. Ninahakika ametumiwa na wavulana wakubwa wa Madrassa. Lazima tuwajue ni kina nani hao.Walimtumia tu!**

**31. LAYLA:** ***(firmly)*** **Lazima awajibike... sote tunafanya hilo- hata mimi!**

**32. HARRY:** **Nakubaliana nawe,lakini usijilaumu.Wacha nipige bongo.Wewe endelea kumtazama Hassan Hospitalini na tutazungumza baadaye tutakapokuwa na muda.**

**33. LAYLA:** **Lakini itawezekanaje kufanya haya yote ikiwa haturuhusiwi kuonana?**

**34. HARRY:** **Tukutane hapa hapa chini ya Daraja-Hapa pako salama. Wewe utajifanya unaenda kufanya mazoezi ya kukimbia. Kisha tutakutane hapa ukiwa pekeyako na kisha urudi nyumbani mbio kabla ya giza kuingia.. sawa? Sasa basi wacha kulia... Najua haitakuwa rahisi kwa babangu mdogo kumsamehe yeyote, lakini Baba anaweza. Yeye ni kiongozi wa jamii.Ni wajibu wake kuisaidia jamii.Futa machozi… tafadhali..!,.**

**35. <u>BRIDGING MUSIC</u>**

**<u>Scene 4. In the village</u>**

**Harry, Chief Dembele**

**36. SFX: Village sounds: birds, cows, goats, chicken**

**FADE IN CONVERSATION**

**37. HARRY:** **Ndio Baba.. nimekuja kutafuta ushauri wako.Tutamsaidia vipi Hassan Omer? Polisi wanamsubiri apate nafuu na kisha wamkamate. Ila najiuliza..kumkamata na kumtenganisha na familia yake mtoto huyu wa miaka 12 kutamsaidia vipi?Msimamo wake unaweza kuwa mkali zaidi.**

**38. CHIEF:** Ungependa nisaidie **vipi?**

**39. HARRY:** **Tafadhali nieleze Baba:Kwani viongozi wa kitamaduni walifanyaje kabla ya sheria na mahakama kuzinduliwa?**

**40. CHIEF:** **Hah! Katika tukio kama hili, tungemuita mhusika na Wazazi wake kwa upande mmoja, na** kwa **upande wa pili watakuwa waliokosewa na katika kisa hiki tungewaita wafuasi wa kanisa, na Babako mdogo Barnabus .Kisha mimi kama jaji, kwa ushirikiano na wazee wa jamii tungezisikiliza pande zote mbili.**

**41. HARRY:** Jee **ungemuadhibu Hassan?**

**42. CHIEF:** **Ehh, wale waliokosewa wangeamua ni adhabu gani wangependa apewe, lakini sisi kama wazee tunaitathmini iwapo inafaa. Kuna sheria maalum na mila,na hadi sasa bado tuna mahakama za aina hii, lakini zinatumika kuzipatanisha jamii zinazozozana.**

**43. HARRY:** **Jee kama Baba mdogo atayatupilia mbali mashtaka hayo itakuwaje? Isitoshe kanisa halikuteketea lote.**

**44. CHIEF:** Ni kweli.Kwa mtazamo wangu H**assan amepata adhabu ya kutosha baada ya kuchomeka mikono**.

**45. HARRY:** **Unafikiri Baba Askofu Baba mdogo atakubaliana na hilo?**

**46. CHIEF:** **Ehh…** ***(pause)*** **Kanisa linahusika moja kwa moja – ni jengo la thamani kubwa.Mbali ya hilo kuna ardhi inayosababisha mvutano baina ya pande mbili.Si mambo mepesi.Hata hivyo mmiliki wa haki atatangazwa na baraza la mandeleo jijini.**

**47. HARRY:** **Na kuhusu uhasama baina ya familia zetu mbili.Utakwisha lini?**

**48. CHIEF:** **Sio tu kwa familia zetu- ni hizi jamii mbili mwanangu..!. Wewe na Layla lazima mjitahidi kuzileta dini hizi mbili pamoja kwenye mdahalo.Niliiandika aya ya Qur'an niliyomsikia rafiki yangu wa Kiislamu akiikariri. Hebu soma hapa… inasema : Mtu anapaswa kuadhibiwa kwa kulipima kosa alilotenda…. Lakini… ahh..ahh.. hii hapa ..**

**49. <u>SFX: Rustle of paper</u>**

**50. CHIEF**: **" Iwapo Mtu atasamehe na alisahau kosa na atake maridhiano ,basi Mwenyezi Mungu atamrehemu.." Na Biblia nayo inasema: "Wanaobarikiwa ni wale wanaodumisha amani. Kwani ni wao ndio watakaouona ufalme wa Mungu"**

**51. BRIDGING MUSIC**

**52. PHILIP/NARRATOR: Wakati huohuo, Mkuregenzi mkuu Bi Milulu, amempendekezea Harry amteue msichana mwengine ayakayekaimu nafasi ya Layla kwa muda,kwani ameomba ruhusu ya wiki mbili.Harry aliliridhia hilo.Nami pia nilikuwepo.Marian Okru ni msichana mrefu, aliye na urembo maalum.Nilitaraji angefanikiwa kumbadili mawazo Harry ili nipate fursa ya kuwa na mpenzi wangu Layla.!**

**<u>Scene 5. Outside – school playground</u>**

**Marian, Harry, Philip**

**53. <u>SFX: Birds, student's voices in the background</u>**

**54. MARIAN: Hatimaye tumekutana tena,Harry.**

**55. HARRY: Ndio Marian, Kundi hili la mjadala na mdahalo halipaswi kusambaratika. Sasa lazima tuanze kujadilia ajenda nyingine ambayo ni "Kwanini baadhi ya wanafunzi hawayapendi masomo ya hesabu na Sayansi?**

**56. MARIAN:** **Ohh, mjadala mzuri sana huo..!, mimi nipo miongoni mwao..kwahiyo nafaa zaidi kuuwasilisha mjadala huu!**.

**57. HARRY:** **Wewe ni miongoni mwao? Kwanini**?

**58. MARIAN:** **Kwa ufupi nafikiri somo la Sayansi linaenda kinyume na maandiko ya mwenyezi mungu.**

**59. HARRY:** **(surprised) Oh! Sawa…...Kwanini unasema hivyo?**

**60. MARIAN:** **Naamini Mungu aliumba mbingu na Ardhi katika muda wa siku saba. Mimi ni mfuasi wa madhehebu ya "Imani Moja ..!."**

**61. HARRY:** **Oh. Jambo la kufurahisha sana hilo. Naamini Mwanadamu aliumbwa ili kutafiti dunia. Na naamini kwamba hii ndio sababu tuko hapa duniani-tutafiti,tuulize maswali na tuyapate majibu yake, na ikiwa yana mafungamano tuchukue hatua zifaazo ,tuyatathmini na tufanye mabadiliko yanayohitajika!.**

**62. MARIAN:** ***(clapping)*** **Sawa tunaweza kuendelea na mjadala huu pamoja na wanafunzi wengine wakati wa mdahalo!**

**63. <u>SFX: Walks away. Footsteps approaching</u>**

**64. HARRY:** **Phew! Oh, Habari Philip!**

**65. PHILIP:** **Labda utahitaji kuwa na subra zaidi Chifu Harry. Lakini ni mrembo au sivyo!**

**66. HARRY:** **Nani?**

**67. PHILIP:** **Marian, nani mwengine-..?Msichana uliyekuwa ukizungumza naye muda mfupi uliopita!**

**68. HARRY:** **(laughing) Oh yule! Hata sikumtia akilini.Kamwe siruhusu maumbile ya mtu yauathiri mtazamo wangu!**

**69. PHILIP:** **Sawa, siku moja nitakukumbusha maneno hayo unayosema!**

**70. HARRY:** **Amani na Ubuntu ndiyo tunayoyahitaji zaidi kwa wakati huu hapa mjini Gori!** ***(Clapping hands) Gonga tano!*** **Ubuntu!**

**71. SIG TUNE UP**

**72. OUTRO:**

**Na hadi kufikia hapo ndipo tunafika mwisho wa kipindi cha leo cha NOA BONGO-Jenga Maisha Yako. Muuguzi Rebecca bado hajakata tamaa kwa Hassan. Naye Harry amejifunza mengi kutoka kwa Babake kuhusu kuwa kiongozi anayejali usawa. Ungana nasi kwa makala yajayo katika mfululizo wa mchezo huu Daraja la Gori ili ufahamu yatakayomsibu Hassan na ikiwa kiranja mpya wa kundi la Mjadala na Mdahalo atafanikiwa kuiteka roho ya Harry.Ukiwa na maoni au ungependa kukisilikiza tena kipindi hiki na vyengine vinavyotayarishwa na Deutsche Welle, tembelea mtandao wetu wa www.dw-world.de/lbe. Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa!**

**END OF EPISODE 6**